For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

Jina.......................................................

Nambari ya Mtahiniwa..............
Nambari ya Usajili....................
Mkondo wa Darasa...................
Sahihi ya Mtahiniwa..................
Tarehe.......................................

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA
Julai/Agosti, 2013
Muda: Saa 2 ½

**102/ 2 Kiswahili P2 – Lugha**
Jumatano 11.00am - 1.30 pm
17/7/2013 (Awamu ya Pili)

**SHULE YA KITAIFA MARANDA**
**MTIHANI WA MWIGO, 2013**
**Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari(Kenya)**

**Maagizo**

(a) *Andika jina lako,nambari ya usajili na mkondo wako katika nafasi ulizoachiwa.*
(b) *Jibu maswali **yote**.*
(c) *Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika karatasi ya maswali.*
(d) ***Karatasi hii ina kurasa 11 zilizopigwa chapa.***
(e) ***Mtahiniwa ni lazima ahakikishe kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | Jumla | |

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Takwimu ambazo zimetolewa na Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO) zinaonyesha kuwa ulanguzi wa watoto umetangaa hususan katika mataifa yanayoendelea. Ipo tumbi ya sababu za kuelezea kwa nini biashara hii imeshamiri.

Athari mojawapo ya utandawazi ni kuunda mtandao mpana ulimwenguni. Mtandao huo unaweza kutumiwa kwa njia chanya au njia hasi. Njia chanya ni zile zinazoweza kuwafaidi wanajamii kwa kuendeleza ubinadamu na kuboresha hali ya maisha kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Maarifa yanayosambazwa huweza kuwa chachu ya kuumua ari ya maendeleo, elimu na mafanikio katika mataifa mengi ulimwenguni. Njia hasi ni zile ambazo maarubu yake ni kuwanufaisha wachache huku zikiwahasiri wengi.

Kuwepo kwa utandawazi kunawapa wenye nia tule, kama vile usafirishaji na ulanguzi wa watoto, fursa ya kuzitosheleza hawaa zao. Wanaoshiriki katika biashara hii huongozwa na uchu wa utajiri. Hawachelei kuwalangua watoto wanaochimbukia mataifa ya kimaskini huko ughaibuni wanakozongomezwa kwenye madanguro, kufanyishwa kazi za sulubu na za kitopasi na kuishi maisha duni.

Asilimia kubwa ya watoto hurubuniwa kwa ahadi ghushi za kujiendeleza kimasomo. Wengine huuzwa kutokana na msaada wa jamaa zao wanaotovukwa na utu na kuwa mawakala katika amali hii ya kusikitisha. Biashara hii huweza kusahilishwa kwa kuwepo kwa mfumo fisadi wa kisheria, msambaratiko wa muundo wa jamaa na ubinafsi wa kijamii.

Ipo haja kubwa ya ushirikiano wa mataifa alkulihali kuikomesha biashara hii haramu. Jamii ya ulimwengu isipofanya hivi, itakuwa imekitia kizazi kitanzi na kuitumbukiza kesho yake kwenye matatizo chungu nzima.

**Maswali**

(a) Ni kwa jinsi gani utandawazi umechangia katika biashara ya ulanguzi wa watoto? (alama 2)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

(b) Eleza jinsi watoto wanaolanguliwa wanavyoishi huko ughaibuni. (alama 3)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

(c) Mwandishi wa kifungu hiki anapendekeza hatua zipi kuchukuliwa ili kusuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto? (alama 4)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

(d) Kulingana na taarifa, kifungu "chachu ya kuumua ari ya maendeleo" kina maana gani? (alama 2)

..................................................................................................................

(e) Jamii isiyosuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto itakuwa na hatima gani? (alama 2)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na taarifa. (alama 2)

(i) maarubu ..................................................................................................

(ii) uchu ......................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Maendeleo ya taifa hutegemea jinsi wananchi wanavyojitolea katika kulibingirisha gurudumu la uchumi wao. Kila mwanajamii anahitaji kujibidiisha katika kazi au taaluma yake. Mzalendo yeyote yule hupata motisha ya kufanya kazi iwapo anaweza kupata ile kazi aliyokuwa akiitamani.

Kumakinika katika taaluma fulani si jambo jepesi na huchukua muda ili kuwepo. Kwa mfano, ili mhazili apate staha ya uhazili sharti apitie ngazi mbalimbali. Mwanzo kabisa lazima ahitimu vyema katika masomo rasmi ya darasani. Masomo hayo pamoja na cheti huweza kumpa fursa ya kujiunga na vyuo mbalimbali vya uhazili. Anapojiunga na vyuo hivyo ndipo safari inapoandaliwa. Kukamilisha safari hii anahitaji muda wa miaka minne -mitano. Anapohitimu, huwa tayari ameimudu shughuli hiyo. Wengi waliokwishapata ujuzi huo wa uhazili huona kuwa hawatapata kazi nzuri yenye mshahara mkubwa. Baadhi yao hujilinganisha na wale wenzao ambao katika masomo wana utaalamu kama wao. Ijapokuwa wote ni wahazili, viwango vyao ni tofauti na mishahara pia hutofautiana. Tofauti hapa ni daraja zao za vyeo. Baada ya kuhitimu na kupata vyeti vya uhazili ni rahisi kupata au kutopata kazi zenye ujira wa kuvutia. Anayefanikiwa katika safari hii hujikakamua hasa kwa upande wa uzingativu wa kazi kikamilifu na kutunza hadhi ya ofisi yake.

Kuna mashirika makubwa yanayojiweza kiuchumi, ambayo raslimali yake ni imara. Mashirika madogo huwa na raslimali yenye kuyumbayumba. Mashirika haya yana wahazili na wafanyakazi ambao hupata mishahara duni. Wafanyakazi hao wote hufanya kazi kwa kutokuwa na uhakika wa kulipwa mwisho wa mwezi. Watu kama hao hawawezi kutilia maanani kazi zao. Mashirika mengine hayana utaratibu maalum wa kulipa mishahara kwa vile hutegemea utu wa mkurugenzi. Baadhi ya wakuu hao huwa na chama cha kupigania haki za wafanyikazi. Wakati wanapotafuta kazi, wahazili wengi huwa ni wahitaji na hukubali chochote wanachopewa.

Wale waliobahatika kupata nafasi ya ajira katika kampuni kubwa za kimataifa, mishahara huwa ni ya kutia moyo. Katika dunia hii wahazili wana vibarua vigumu kwa sababu lazima wapate tajriba na uzoefu wa taaluma inayoendelezwa na shirika fulani. Mhazili sharti azoee istilahi zinazotumiwa. Wakurugenzi mara nyingi hukosa kuwa na subira. Mhazili anapotumia msamiati usioenda sambamba na mahitaji ya wakurugenzi kama hao, basi hurushiwa matusi ya kila aina. Wavumilivu miongoni mwao hula mbivu. Hawa hawafi moyo bali hujitahidi zaidi ili wasikumbwe na kimbunga cha kufokewa. Kuna wengine ambao humwaga unga kutokana na makosa madogo madogo.

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa, fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno baina ya (45-50) (alama 6, utiririko 1)

**Matayarisho**

**Jibu**

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(b) Kwa kuzingatia aya mbili za mwisho, eleza kwa maneno baina ya (55-60) masaibu yanayowakumba wahazili. (alama 9, utiririko 2)

**Matayarisho**

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

**Jibu**

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

3. **MATUMIZI YA LUGHA** **(ALAMA 40)**

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(a) Taja ala zinazohusika kutamkia neno **ghali**. (alama 2)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(b) Tambua mzizi katika fungutenzi hili: **Anaomboleza**. (alama 1)

..............................................................................................................

(c) Bainisha viambishi nafsi viambata katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Niliwafukuza walevi hao na kumsaidia mzee huyo, akashukuru.

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(d) Andika neno moja lenye silabi mwambatano ya konsonanti mbili. (alama 1)

..............................................................................................................

(e) Kanusha: (alama 2)

Najojo amemaliza kupika chakula ambacho kingalikuwa chake angalifurahi sana.

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(f) Hii ni sentensi aina gani? Toa sababu. (alama 2)

Yule na Mwanasura hawakufika nyumbani jana.

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(g) Tumia kiambishi –ni- katika sentensi kuonyesha hali(umri) (alama 1)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(h) Dunisha kwa umoja. (alama 2)

Ngozi za wasichana hawa wafupi ni laini.

..................................................................................................

..................................................................................................

(i) Andika upya sentensi ifuatayo ukitumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 3)

Kuvunjika kwa ndoa husababishwa na unywaji mwingi wa pombe pamoja na uzinifu.

..................................................................................................

..................................................................................................

..................................................................................................

..................................................................................................

(j) Eleza matumizi ya 'kwa' katika sentensi: (alama 2)

Nilipomwona kwa macho, nilimwadhibu kwa kuiba kalamu yangu.

..................................................................................................

..................................................................................................

..................................................................................................

(k) Ainisha nomino katika tungo hili. (alama 2)

Ufundi wake ulimwezesha kupata bunda la noti lililopotea.

..................................................................................................

..................................................................................................

..................................................................................................

..................................................................................................

(l) Tumia 'o' rejeshi tamati kuunganisha sentensi hizi. (alama 2)

i. Mtoto yule ni mwenye heshima.

ii. Mtoto yule anacheza vizuri sana.

..................................................................................................

..................................................................................................

..................................................................................................

..................................................................................................

..................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(m) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Wafanyakazi watakaokaidi amri ya Waziri wa Leba watachukuliwa hatua kali.

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(n) Vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi hii viko katika kauli gani? (alama 2)

Ng'mbe ambaye alikwama shimoni hapeki chakula.

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(o) Changanua kwa kutumia matawi. (alama 4)

Mama mpole ajabu aliyepigwa na mumewe ni daktari bora.

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(p) Sahihisha: (alama 1)

Serekali haijatimiza ahadi yake kwa walimu juu haina pesa.

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(q) Huku ukitoa mifano, andika matumizi matatu ya kistari kifupi. (alama 3)

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

(r) Geuza sentensi ifuatayo kwa wakati uliopita, hali endelevu. (alama 2)

Ninapolima, yeye hunipongeza.

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

(s) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)

" Hawa wote ni wahalifu kwani waliniibia pesa jana na kudokeza kuwa wataendelea na wizi huu hadi nihame." Mapesa alijitetea.

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

(t) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii. (alama 2)

Wanaoishi mashambani wanaogopa polisi zaidi ya simba.

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

4. **ISIMUJAMII** **(ALAMA 10)**

Lugha hutumika kama chombo cha mawasiliano katika jamii. Hata hivyo, baadhi ya lugha hufifia huku nyingine zikichipuka. Eleza sababu tano zinazopelekea hali hii kutokea. (alama 10)

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................